# Learning by Ear 2009
# Children's Rights Series
# 01 Child soldiers

**Topic:** **Children in times of war**

**Author:** **Adrien Demun (Uganda)**

**Kisuaheli:** **Eric Ponda**

**!! NB: PSEUDONYM = Henri Leenhart!!!!!**

**Editor:** **Sandrine Blanchard**

**Translator:** **Anne Thomas**

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| IN/OUTRO | X | | Unimportant | |
| Narrator | | X | Ca. 25 | |
| Kisembo Mukisa | | X | 20 | Lingala |
| Umirembe | | X | 20 | Lingala |
| Faustin | | X | adult | French |

| LbE Soundtrack |
|---|

**INTRO:**

Hujambo msikilizaji na karibu kwa awamu nyingine ya mfululizo wa vipindi vya "Noa Bongo Jenga Maisha yako", ambapo mara hii tunaangazia suala la haki za Watoto na juhudi za kudumisha amani.

Leo tanazungumzia masaibu yanayowakumba watoto hasa wakati wa vita, na moja kwa moja tunaelekea nchini Uganda tunakokutana na Vijana wawili, Kisembo na Umirembe. Vijana hawa walikuwa maadui wakubwa, lakini matatizo ya dunia yamewaleta pamoja na kuwa dhamira moja maishani. Wote walikuwa kuhudumu wanajeshi watoto. Wakiwa na umri huo mdogo, vijana hawa walijikuta katikati ya mizozo ya kivita wasioijua chanzo chake. Wameshuhudia udhallimu na hata wao wenyewe kutekeleza vitendo vya ukatili wakiwa jeshini, ambavyo daima wanakiri vitasalia kumbukumbu maishani mwao..

**REPORT**

**1. Atmo pool**

**Narrator:**

Tumekubaliana tukutane katika orofa ya kwanza ya mkahawa unaomilikiwa na raia wa Lebanon mjini Kampala. Kisembo Mukisa na Umirembe ni mabarobaro wa umri wa miaka 20 sasa. Unapokutana nao kwa mara ya kwanza, huwezi hata kidogo kudhania ni watu tofauti na mabarobaro wengine. Wanaonekana wapole, wanyenyekevu na wenye nidhamu zao. Lakini kinyume kabisa Kisembo na Umirembe wamepitia mengi maovu na ya ukatili. Hawakuwa wametimu umri wa miaka 14 waliposhirikishwa katika vita vikali zaidi vya kikabila miaka 10 iliyopita.Vita baina ya makabila mawili, lile la Lendu ambalo ni kabila la wakulima waliohamia kutoka nchini Sudan na Wa-Hema, ambao ni

wafugaji wa kuhamahama kutoka nchini Uganda, na sehemu za Kusini Mashariki mwa Ethiopia. Vita hivyo vilitokea kati ya mwaka wa 1998 na 2003 katika jimbo la Ituri mashariki kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Kisembo Mukisa anakumbuka siku ujana wake ulivyokatizwa ghafla.

**2. Kisembo** (int. 1 – lingala) :
"Nillikuwa nimetoka matembezi na marafiki zangu mjini. Niliporejea nyumbani nikakutana na majirani walioniarifu kwamba nyumba yetu imevamiwa na majambazi kutoka kabila la Walendu na kuwaua kinyama Babangu, Mamangu na Dadangu mdogo"

**Narrator:**
Kisembo alishikwa na woga na kutorokea kichakani. Kufikia mwaka wa 2002 alipokuwa na umri wa miaka 13, tayari vita baina ya makabila hayo mawili vilikuwa vimedumu kwa muda wa miaka 4, na bado vilikuwa vinaendelea kupamba moto----kufuatia hatua ya seriakli ya Uganda kulikalia eneo hilo. Kabla ya Kisembo kupoteza familia yake, hakuona maana ya vita hivyo, lakini baada ya mauaji hayo ya mwaka wa 2002, Kisembo alibadili nia na hapo akashika njia kuelekea Musipela--- ngome ya kabila la Hema katika eneo la Bunia, makao makuu ya jimbo hilo la Ituri. Hasa lengo lake kubwa lilikuwa kupata usaidizi wa kulipiza kisasi mauaji hayo.

**ATMO**

Na bila kupoteza wakati, Kisembo akajiunga na kundi la wapiganaji la Union of Congolese Patriots- UPC, kundi la kisiasa lililojihami likiongozwa na mbabe wa kivita Thomas Lubanga, ambaye sasa anakabiliwa na mashtaka katika mahama ya kimataifa kwa kosa la kuwasajili watoto katika makundi ya kivita. Wakati huo alikuwa akiungwa mkono na serikali ya Uganda na Rwanda. Kisembo anakumbuka shughuli ya kuwasajili watoto jeshini ilikuwa jambo la kawaida:

**3. Kisembo** (int. 2 lingala) :
"Nilipowasili Musipela, nilikutana na wapiganaji wengi sana. Walinieleza kwamba wameamua kujiunga na kundi hilo la UPC kwa sababu wanatoka kabila la Lendu, na wana jukumu la kutekeleza. Si mapenzi yao wakasema "

**Narrator:**

Kisembo alipelekwa hadi kambi ya mafunzo ya kijeshi ya Mandro – yapata umbali wa kilomita saba kutoka Bunia.

**4. Kisembo** (Int. 3 lingala) :
"Tulipitia mateso mengi. Maisha yalikuwa magumu sana. Tulilazimika kula chakula kibovu na hatungeweza kulala katika vibanda tulivyotengewa. Maisha yalikuwa magumu!Tulilazimishwa kufanya mazoezi ya kukimbia na kuimba kila alfajiri na mapema kwa masaa kadhaa. Tulifanya kazi zote za nyumbani. Kwa mfano kutafuta kuni vichakani. Na tunaporejea tunapewa chakula kisichofaa kabisa. Mara nyingine tulikuwa tunapumzika mwendo wa saa tisa usiku kwa saa moja,

kisha tunaendelea na mazoezi ya kukimbia, na kuimba usiku kucha. Hatukupata muda wa kutosha kulala, na mara nyingine tuliamshwa usiku wa manane kuendelea na mazoezi hayo"

**Narrator:**
Lakini ingawa maisha katika kambi hiyo ya Mandro yalikuwa magumu hayawezi kulinganishwa na ukatili uliofuatia. Huyu hapa tena Kisembo:

**5. Kisembo** (Int. 4 lingala) :
« Wakati mmoja wetu anapofanya makosa makubwa, adhabu yake ilikuwa ni kufungwa kamba kwenye mti na kisha kuuawa kwa kupigwa risasi. Lakini kwa wale wa makosa madogo waliadhibiwa kwa kuchapwa viboko na makurutu wengine."

**Narrator:**
Kisembo hakuiba silaha wakati wote wa mafunzo ya mwezi mmoja na nusu. Wala hakujaribu kutoka kambini. Kwa hivyo hakupata adhabu iliyowapata wengine. Badala yake alituzwa kwa bunduki aina ya AK 47 na kisha yeye na watoto wengine kutoka kabila hilo la Hema kuamriwa kwenda kuvamia vijiji vya Wa-Lendu

**6. Kisembo** (Int. 5, lingala) :
"Kamanda wa oparesheni, Bosco Ntaganda, alikuwa akituamrisha na kutuelekeza katika kijiji cha Wa-Lendu kinachopasa kushambuliwa. Maagizo tuliyopewa ni kuua bila ya kuuliza yoyote tunayekutana."
"Kwanza tuliwaua Wa-Lendu wote tuliokutana nao mjini Bunia. Kisha tukaelekea vijijini kama vile Zumbe na Songolo."

**7. Atmo pool**

**Narrator:**

Kundi la wapiganaji alilojiunga nalo Kisembo, halikutaka kumnusuru mtu yeyote ambaye si kutoka kabila lao. Yaaminika raia takriban 800 waliuawa na kundi la UPC katika eneo la Mongbwalu pekee kati ya mwaka wa 2002 na 2003. Kwa mujibu wa Redio Okapi, inayomilikiwa na Umoja wa mataifa katika eneo hilo, Thomas Lubanga alitoa agizo la kila familia inayoishi katika himaya yake lazima iunge mkono juhudi za kundi hilo kwa kutoa mifugo, pesa au watoto kujiunga nalo kama wapiganaji. Makundi ya maadui pia yalikuwa na muongozo huo huo, kuchoma nyumba na kuuwa watu kinyama. Mauaji hayo ya jimbo la Ituri yalisababisha maelfu ya raia kuyahama makaazi yao wakitoroka vita hivyo.

**7. ATMO pool**

Umirembe, ambaye tulikutana naye akicheza mchezo wa Pool na mwenzake Kisembo mjini Kampala, alikuwa na umri wa miaka 12 alipotekwa nyara na wapiganaji wa Kilendu wakati akitoka shuleni. Ilikuwa mwaka wa 2000 na hapo moja kwa moja akapelekwa katika kambi ya kijeshi.

**8. Umirembe** (int. 6, lingala) :

"Maisha yalikuwa magumu sana. Tulifanya mazoezi magumu. Kukimbia na kadhalika. Kisha kuamriwa kwenda vijijini kuwateka nyara

wasichana wadogo na kuwaleta kwa wakubwa wetu waliowatumia kimapenzi. Pia sisi tulikuwa tukiwabaka."

**Narrator:**

Oparesheni ya kundi la wapiganaji wa kabila la Lendu ilipamba moto:

**9. Umirembe** (Int. 7, lingala)
"Tulivishambulia vijiji vya Wahema mjini Bunia kama vile Bogor, Tchey, vijiji vyote vya Wahema. Tuliamriwa tukimuona Muhema kijijini au hata barabarani atuonyeshe mali yake yote na kisha baada ya kuipora tumuue. Pia tulikuwa tukiwaona wasichana tunawabaka na kisha kuwaua kama  Wahema wengine"

**Narrator:**

Mwaka wa 2003, Wapiganaji wa  kundi la Hema waliingia katika kijiji cha Bogoro anakotoka Umirembe na kuua familia yake baada ya kumbaka Mamake. Umirembe alitorokea msituni ambako alijificha kwa muda wa miaka miwili.

Wakati huo huo , Kisembo, akiwa mototo mwanajeshi katika kundi la wapiganaji wa Kihema,  aliamua kutoroka jeshini na kuwa raia wa kawaida miongoni mwa jamii ya Wa-Congo. Aliweza kunufaika na mradi wa kuwapokonya silaha makundi ya wapiganaji ulioanzishwa mwaka wa 2004. Alilipwa ruzuku ya kiasi cha Dola 100 na Umoja wa mataifa baada ya kusalimisha silaha yake.

**10. Kisembo** (Int. 8, lingala)
"Nilifungua duka dogo mjini. Lakini tatizo ni kwamba si wapiganaji wote waliosalimisha silaha zao. Baadhi yetu walijiunga na jeshi la taifa wakiwa na silaha zao. Mara Nyingine walikuja wakati wa usiku kupora mali mjini. Siku moja walinivamia na kunifunga kwenye gunia kabla ya kupora mali yangu yote."

**Narrator:**

Akiwa amechoshwa na maisha ya kuishi peke yake bila fedha, Kisembo aliamua kuvuka mpaka kupitia ziwa Albert, ili kujaribu bahati yake nchini Uganda. Huko alikutana na wakimbizi wengi raia wa Congo wanaoishi mjini Kampala akiwemo Faustin Katanga. Katanga alikuwa inspekta wa Polisi mjini Bunia lakini alilazimika kutoroka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo wakati wa vita hivyo, kwa sababu alifahamu mengi kuhusu watu waliokuwa hatari kwa usalama. Bado anakumbuka shughuli ya kuwasajili watoto jeshini:

**11. Faustin** (Int. 9) frz.:
" Wababe wa kivita walianza kuwasajili watoto. Ilikuwa dhahiri kwamba kila kabila lilikuwa likishambuliwa. Watoto, wasichana kwa wavulana walijiunga na makundi hayo ya wapiganaji ili kulipiza kisasi"

**Narrator:**

Shughuli hiyo ya kuwasajili watoto jeshini ilifanyika wka mpango maalum na ikawa ni lazima. Anasema Faustin Katanga:

**12. Faustin** (Int. 10) frz. :
"Kwanza kabisa,yalikuwa makundi ya kujitolea katika pande zote mbili. Lakini kisha baadaye yakaanza kuwalazimisha baadhi ya wazazi ambao walikataa watoto wao kujiunga na makundi haya. Hata hivyo walichukuliwa kwa lazima. Wakati mwengine tulipokuwa tukiwatarajia watoto wetu warudi nyumbani kutoka shuleni, tunasikia wako katika kambi ya wapiganaji ya Mandro au Sota- hizo zilikuwa kambi za wapiganaji wa kundi la Hema. Au unasikia wako Ngéti – kambi za wakipiganaji wa Ki-Lendu. Hivyo ndivyo ilivyokuwa.

**Narrator:**

Vita hivi vya kikabila vilichochewa na mataifa jirani kama vile Uganda na Rwanda. Nchi hizi zilihusika kwa namna moja au nyingine katika vita hivi. Mashirika mengi yasiyo ya kiserikali yalilaani vikali kitendo hiki. Ripoti ya mwaka wa 2003 ya shirika la madaktari wasio na mipaka ilitaja uhasama baina ya nchi hizi kutaka kulidhibiti eneo hilo kisiasa na kupora rasilimali katika eneo hilo kuwa chanzo cha kuendelezwa kwa vita hivyo. Shirika la UNESCO lilisema kwenye ripoti yake kwamba Uganda na Rwanda zilitaka mipaka ya nchi hizo iliyorithiriwa kutoka kwa wakoloni uchunguzwe upya ili nazo ziweze kunufaika na rasilimali zilizoko katika jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Kisembo Mukisa anakumbuka majukumu ya kuchukiza yaliyotekelezwa na nchi jirani:

**13. Kisembo** (Int. 11) :

"Jeshi la Uganda lilikuwepo lakini lilikuwa kama ndumakuwili .Lilitupatia silaha kushambulia mji wa Bunia huku kwa upande mwengine likiwapa silaha wapiganaji wa Ki-Lendu kutushambulia."

**Narrator:**

Wakiwa uhamishoni mjini Kampala Vijana hawa waliokuwa wapiganaji utotoni wanaishi maisha ya raha mstarehe. Mara nyingine kutokana na msaada kutoka kwa marafiki zao au makundi ya maoni kanisani kuwasaidia.

Lakini wachochezi wa vita katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo hawajaweka silaha chini. Mnamo mwaka wa 2008 makundi mawili kati ya saba ya wapiganaji yalikuwa bado yakiendesha harakati zao. Wapiganaji 25,000 na watoto 11,000 walikuwa wamepokonywa silaha. Ndio sababu Umoja wa mataifa ukaanzisha mpango wa huduma za binadamu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo huku asilimia 10 ikitengewa jimbo la Ituri. Mpango huu ulikusudiwa kuwafanya wapiganaji 15,000 wanaoendelea kuwasajili watoto jeshini kusalimu amri.

Bosco Ntaganda ni mkuu wa kundi la wapiganaji la UPC lililobuniwa na Thomas Lubanga . Bado anaendelea kuwasajili watoto jeshini licha ya kushtakiwa katika mahakama ya kimataifa . Kisembo Mukisa:

**14. Kisembo** (Int. 12, lingala) :
"Mapambano bado yanaendelea. Usajili wa watoto jeshini pia bado unaendelea hadi sasa japo kwa siri. Kuna baadhi ya watu mjini Kampala

ambao wamepewa kandarasi ya kuwasajili watoto jeshini. Ni kama biashara siku hizi."

**Narrator:**

Lakini Kisembo Mukisa na Umirembe hawana mipango ya kujiunga tena na makundi ya wapiganaji. Vita kwao vimekwisha. Lakini machungu waliyonayo ni mengi mno na ndio yameanza.
Kisembo Mukisa.

**15. Kisembo** (Int. 13, lingala) :
"Kusamehe tunaweza kusamehe….Lakini machungu niliyonayo kutokana na mauaji ya kinyama yaliyotekelezwa kwa familia yangu daina yatabaki doa moyoni"

**Narrator:**

Kati ya mwaka wa 2002 na 2003, zaidi ya watu 8,000 waliuawa kinyama katika jimbo la Ituri na wengine zaidi ya 800,000 kuyahama makaazi yao. Tume ya kulinda amani ya Umoja wa mataifa nchini Kongo, MONUC, ilitangaza mnamo mwaka 2004 kwamba haya ni mojawapo ya mauaji mabaya zaidi kuwahi kutokea Duniani"

**End music**

**OUTRO :**

Na hadi hapo ndipo tunafika mwisho wa r inayotukamilisha kipindi chetu cha leo. Kipindi hiki kimeandaaliwa na Henri Leenhart kutoka mjini Kampala Uganda. Unaweza kusikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao; tovuti yetu ni www.dw-world.de/lbe. Ungana nasi tena wakati mwingine kwa makala mengine. Hadi wakati huo, kwaheri kwa sasa!

**Music**